



YAH: HUDUMA YA UCHUNGUZI WA SARATANI

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WA WILAYA YA MISUNGWI KWAMBA, KATIBU TAWALA MKOA WA MWANZA KWA KUSHIRIKIANA NA MADAKTARI BINGWA WA HOSPITALI YA RUFAA YA KANDA YA BUGANDO, KWA PAMOJA WATAFANYA ZOEZI LA UCHUNGUZI WA VIVIMBE VYA SARATANI KATIKA MATITI NASEHEMU NYINGINE ZA MWILI KWA WANANCHI WOTE.

ZOEZI NA HUDUMA HII ITATOLEWA SIKU YA ALHAMISI TU, TAREHE MOJA MWEZI WA KUMI, MWAKA HUU 2020, KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA MISUNGWI KUENZIA SAA MOJA ASUBUHI HADI SAA KUMI KAMILI JIONI.

EWE MWANANCHI KUMBUKA KWAMBA HUDUMA YA UCHUNGUZI HUU ITATOLEWA BURE (HAKUNA MALIPO YOYOTE)UNAOMBWA KUJITOKEZA ILI KUTAMBUA TATIZO NA HATIMAYE KUPATA MATIBABU.

EWE MWANANCHI, EWE BABA, EWE MAMA, EWE MTOTO ULIYE NA UVIMBE WOWOTE MWILINI JITOKEZE ILI UWEZE KUPATA UCHUNGUZI NA VIPIMO NA BAADAE KUPATIWA MATIBABU.

KUMBUKA SERIKALI IMEAMUA KUMKOMBOA MWANANCHI DHIDI YA MAGONJWA YA SARATANI HIVYO, BASI TUNAOMBA TUUNGANE, TUPAMBANE, TUSONGE MBELE ILI TUMWOKOE MWANANCHI.

USIKIAPO TANGAZO HILI MJULISHE NA JIRANI YAKO.

LIMETOLEWA NA:

KISENA MABUBA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MISUNGWI

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MISUNGWI**